

# Waliobadili matumizi ya ranchi kikaangoni

>>Uk.5 **WAWEKEZAJI waliobadili matumizi ya ardhi ya vitalu walivyopewa kwenye maeneo ya ranchi za taifa wako mbioni kunyang'anywa baada ya...**



Scanned with CamScanner

# Waliobadili matumizi ranchi za Taifa kikaangoni

**Bakari Kiango**, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ametoa siku kumi kwa Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco) kubaini na kuwanyang'anya maeneo wawekezaji waliopatiwa vitalu kwenye ranchi za taifa na kubadili matumizi ya ardhi kinyume na makubaliano ya mikataba yao.

Ndaki alieleza hayo juzi hayo wakati alipotembelea ranchi ya Usangu iliyopo wilayani ya Mbarali mkoani Mbeya kisha kufanya mkutano wa hadhara na kufanya mkutano wa hadhara na baadhi ya wawekezaji, wakulima na wafugaji wanaofanya shughuli zao katika ranchi hiyo.

Taarifa iliyotolewa jana na wizara hiyo ilieleza kuwa katika ziara hiyo, Ndaki alibaini baadhi ya wawekezaji waliopatiwa vitalu na Narco kwa ajili ya kufuga na kulima malisho ya mifugo wamekuwa wakikodisha maeneo hayo kwa wakulima na wafugaji kinyume na mkataba.

"Siku 10 nadhani zinawatosha kubaini watu wanaojiita wawekezaji, waliobadilisha matumizi ya ardhi ambayo siyo kufuga wala malisho wanyang'anywe maeneo kwa kuwa wameenda kinyume na utaratibu wa mkataba kati yao. Nitafuatilia na nitapenda kupata taarifa mmepata wangapi na wangapi wamenyang'anywa," alisema Ndaki.

Ndaki alilazimika kutoa kauli

**2mil**
Fedha wanazolipa wafugaji kwa kukodisha hekari moja kwa miezi minne.

**10**
Siku walizopewa Narco kuwabaini watu waliobadili matumizi ya ardhi.

hiyo baada ya kupata taarifa kutoka kwa baadhi ya wakulima na wafugaji wa Mbarali kuwa wamekuwa wakikodishwa maeneo ya ranchi hiyo na wawekezaji kwa Sh 20,000kwa hekari moja kwa ajili ya kilimo kisha kutoa madebe 10 ya nafaja baada ya mavuno.

Wakati wakulima wakitoa hayo, wafugaji wamekuwa wafugaji wakilipa Sh 2milioni kwa hekari moja katika kipindi cha miezi minne kwa ajili ya kulisha mifugo yao katika maeneo ya wawekezaji waliopatiwa vitalu na Narco kwa ajili ya kulima malisho au kufuga.

Pia ameutaka uongozi wa Narco ifikapo Februari 15uongozi wa kampa wawekezaji waliolipa na wasiolipa madeni ili wachukuliwe hatua akisema hadi sasa taasisi hiyo inawadai wawekezaji zaidi ya Sh8bilioni.



Scanned with CamScanner




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akisalimiana na baadhi ya wakulima na wafugaji wanaofanya shughuli zao kwenye Ranchi ya Usangu iliyopo Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waziri aagiza wakulima wapewe ranchi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Profesa Elisante Ole Gabriel, kuandaa utaratibu mzuri wa kukodisha mashamba ya malisho (banchi) kwa wakulima ambayo wako tayari kulipa kodi ya mashamba hayo kwa serikali.

Ndaki alitoa agizo hilo jana alipohitimisha ziara yake ya siku mbili mkoani Mbeya, akitembelea eneo la ranchi ya Usangu iliyoko wilayani Mbarali na kuzungumza na wakulima na wafugaji kujua vikwazo vinavyowakabili.

Wakulima wa Bonde la Usangu walimweleza Waziri Ndaki kuwa kwa sasa wanakodisha mashamba ya ranchi kutoka kwa wawekezaji na kwamba gharama ni kubwa, hivyo waliomba serikali kuwamegea eneo lao kwa ajili ya kilimo.

Mmoja wa wakulima hao, Pascalina Mhagama, alisema ekari moja ya shamba wanakodishiwa Sh. 50,000 na kwamba baada ya mavuno, hutakiwa kutoa kiasi cha mpunga wanaovuna kwa wawekezaji hao.

Alisema hali hiyo inawaumiza, hivyo wanaiomba serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), kumega baadhi ya maeneo ya ranchi ili yatumike kwa ajili ya kilimo.

Kutokana na malalamiko hayo, Waziri Ndaki alielekeza kuwa maeneo yote yaliyoshindwa kuendelezwa kwa ajili ya malisho ya mifugo, yakodishwe kwa wakulima ili kuleta mapato kwa serikali.

Alisema kwa sasa wawekezaji wengi wana malimbikizo ya madeni na hivyo wanyang'anywe maeneo hayo na wakodishiwe wakulima ambao watakuwa wanalipa fedha kwa serikali.

"Ranchi ya Usangu ina jumla ya vitalu 16, lakini ukifuatilia vitalu hivi havifanyi kazi kwa mujibu wa mkataba, ni maalum kwa ajili ya malisho ya mifugo badala yake wameamua kuwakodishia wakulima na wanachukua fedha ambazo serikali hainufaiki nazo.

"Licha ya kuchukua fedha kutoka kwa wakulima, bado wana madeni. Sasa ninaagiza vitalu vyote vilivyoshindwa kutimiza masharti ya mkataba, vikodishwe kwa wakulima ili serikali iendelee kupata fedha," aliagiza.

Akipokea maelekezo hayo, Katibu Mkuu Profesa Ole Gabriel alisema atafanya mazungumzo na Katibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuangalia namna bora ya kugawa maeneo hayo ya ranchi nchini, yaanze kutumika kwa ajili ya kilimo.

Alisema suala hilo litashughulikiwa na kuwatoa hofu wakulima walioomba kuwa watapewa na kuwahakikishia kuwa wawekezaji walioshindwa kulipa madeni ya NARCO, lazima wataondolewa.

Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Francis Mtega, alisema ardhi ya Mbarali ni ndogo kulinganisha na mahitaji ya wakulima, wafugaji na wawekezaji.

Aliomba serikali kuandaa utaratibu mzuri wa kugawa maeneo hayo ili kila kundi linufaike na ardhi hiyo na kuepusha migogoro ya mara kwa mara baina ya wafugaji na wakulima.

Aliwataka wawekezaji kuwa waaminifu na kulipa madeni yote wanayodaiwa na serikali na kwamba kwa kufanya hivyo, kutaongeza mapato na huduma za jamii zitaendelea kuboreshwa.

Scanned with CamScanner

# Livestock minister urges PS to come up with plan allowing farmers to use raches owned by state

**By Guardian Correspondent, Mbarali**

LIVESTOCK and Fisheries Minister Mashimba Ndaki yesterday directed the permanent secretary, Prof Gabriel Ole Sante to come up with a plan that will allow farmers to hire state-owned ranches for agricultural activities.

Minister Ndaki made the statement when winding up his two-day official tour in Mbeya Region. The minister also visited the Usangu ranch in Mbarali District where he held meetings with farmers and livestock keepers.

During the meetings, farmers informed the minister that they have been leasing farms within the ranch, but contracts are signed between them and the investor. They requested the government to put in place an arrangement where they can directly hire the farms from the government.

Representing farmers, Pascalina Mbagama told the minister that they have been hiring one acre at a cost of 50,000/-, adding that after harvesting each of the farmers are also required to give the investor 300 kilos of rice.

"We would be grateful if the government through the National Ranching Company Limited (NARCO) gives us part of the ranches for commercial farming activities," she said.

Responding to farmer's concerns, minister Ndaki directed that all the undeveloped farms and ranches should be given to small scale farmers for production of cash and food crops. He added that empowering small scale farmers would also boost government revenues.

He said most of the investors in state-owned ranches have not paid their debts, insisting the ranches must also benefit small scale farmers.

"The Usangu ranch has a total of 16 blocks, but most of them are not operating as per agreement; investors are leasing the farms to small scale farmers instead of developing them," said the minister.

The PS assured the minister that all the directives will be implemented and that he will soon consult the Minister for Lands, Housing and Human Settlements Development on how to demarcate the investor's ranches and farms.

Ole Sante assured farmers that all the undeveloped farms and ranches will be given to them as soon as the government finalises all the required procedures.

He urged investors to clear their outstanding debts at NARCO threatening to terminate the contracts.

Mbarali Member of Parliament, Francis Mtega said the district has a limited agricultural land compared to the population which includes farmers, livestock keepers and investors.

"There should be an arrangement which will not only benefit the investors, but all residents. This would also reduce complaints as well as land disputes between farmers and livestock keepers," said the legislator.

> **"The Usangu ranch has a total of 16 blocks, but most of them are not operating as per agreement; investors are leasing the farms to small scale farmers instead of developing them**



Scanned with CamScanner

Habari Leo 14 Jan 2021, Uk 8

# Waziri atoa mwezi NARCO walipwe bilioni 6/-



**Na Mwandishi Maalumu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ametoa mwezi kwa wawekezaji kulipa malimbikizo ya deni la Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco) ambalo ni zaidi ya Sh bilioni 6.

Waziri Ndaki ameutaka uongozi wa Narco kufikia Februari 15, mwaka huu, saa saba mchana awe amepata taarifa ya wawekezaji waliolipa madeni yao na ambao hawajalipa, kabla ya kuchukuliwa kwa hatua zaidi.

"Wawekezaji wote ambao tunawadai hapa Usangu na kwenye ranchi zingine wote walipe pesa ya Narco tulipokubaliana kwenye mkataba tulikubaliana mtalipa pesa, mlipe madeni yenu ifikapo tarehe 15 mwezi Februari saa saba mchana," alisema Ndaki.

Aliongeza, "Tunataka Narco ijiendeshe kibiashara, lakini sioni tukielekea kwenye kujiendesha kibiashara na moja ya matatizo yanayotufanya tusifike huko ni kulea watu wa namna hii."

Alisema wale ambao hawatakuwa wamelipa hadi kufikia muda huo wanyang'anywe maeneo hayo ili wapatiwe watu wengine ambao watalipa kwa mujibu wa mkataba ili Narco ifikie malengo yake na kulalamika kuwa Narco imechelewa kuchukua hatua kwa watu ambao wamekuwa na madeni ya siku nyingi.

Alisema wizara imefanya tathmini juu ya madeni hayo na kuagiza yalipwe katika viwango na tozo mpya zilizowekwa kwa sababu imejiridhisha kwamba kwa gharama hizo Narco itajiendesha na kuhudumia vizuri ranchi zake.

Kwa mujibu wa taarifa ya Narco iliyotolewa na Kaimu Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Masele Mipawa, maeneo ya vitalu katika ranchi za taifa yanayokodishwa kwa wawekezaji yamegawanywa katika viwango vitatu.

Alivitaja kuwa ni kiwango cha chini ni Sh 3,500 kwa ekari moja kuanzia eneo lenye hekta moja hadi 2,000, kiwango cha kati ni Sh 5,500 kwa ekari moja kuanzia eneo lenye hekta kuanzia hekta 2,001 hadi 5,000 na kiwango cha juu ni Sh 7,500 kwa ekari moja kuanzia eneo lenye hekta zaidi ya 5,001.

Aidha, Ndaki alimuagiza Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuangalia namna ya kukodisha maeneo ya ranchi za taifa kwa wakulima ambao wanaweza kulima malisho ya mifugo ili kuondokana na migogoro ya wakulima kupata maeneo kwa ajili ya kilimo ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema ni muda muafaka kwa wizara kuangalia namna wananchi wanavyoweza kutumia maeneo hayo kwa tija kwa taifa badala ya kusubiri wawekezaji ambao baadhi yao wamekuwa wakienda kinyume cha makubaliano ya mikataba na kuwafanya wananchi wanaoishi karibu na ranchi za taifa kukosa maeneo ya kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Katibu Mkuu (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel alisema atasimamia maelekezo yote yaliyotolewa na waziri likiwemo la wawekezaji kulipa madeni ya vitalu walivyokodishwa ili Narco inayomiliki maeneo hayo ijiendeshe kibiashara kama moja ya malengo ya kampuni hiyo kupitia maeneo yake.

Scanned with CamScanner




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (katikati), Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel ( wa pili kushoto kwake) na baadhi ya wakulima na wafugaji wanaofanya shughuli zao kwenye Ranchi ya Usangu iliyopo wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya na baadhi ya wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi hiyo. Waziri Ndaki amemaliza ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani Mbeya kwa kuwataka wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi za taifa kuheshimu mikataba waliyoingia na kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO). (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

Scanned with CamScanner

# Waliokaidi mkataba wa NARCO kikaangoni

Na Edward Kondela

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ametoa siku kumi kwa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kubaini na kuwanyang'anya maeneo, wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi za taifa ambao wamebadili matumizi ya ardhi kinyume na makubaliano ya mkataba yao.

Waziri Ndaki amebainisha hayo juzi wakati alipotembelea Ranchi ya Usangu iliyopo Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya alipokuwa kwenye ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani humo na kufanya mkutano wa hadhara na baadhi ya wawekezaji, wakulima na wafugaji, ambao wanafanya shughuli zao katika ranchi hiyo na kubaini kuwa baadhi ya wawekezaji waliopatiwa vitalu na NARCO kwa ajili ya kufuga na kulima malisho ya mifugo wamekuwa wakikodisha maeneo hayo kwa wakulima na wafugaji kinyume na mkataba.

"NARCO siku kumi nadhani zinawatosha kubaini watu wanaojiita wawekezaji, waliobadilisha matumizi ya ardhi ambayo siyo kufuga wala malisho wanyang'anywe maeneo kwa kuwa wameenda kinyume na utaratibu wa mkataba kati yao na NARCO, na mimi nitafuatilia nitapenda kupata taarifa mmepata wangapi na wangapi wamenyang'anywa kwa kuwa wameenda kinyume na utaratibu waliokubaliana" alisema Ndaki.

Waziri Ndaki amelazimika kutoa kauli hiyo baada ya kupata taarifa kutoka kwa baadhi ya wakulima na wafugaji wa Wilaya ya Mbarali kuwa wamekuwa wakikodishwa maeneo ya ranchi hiyo na wawekezaji kwa shilingi 20,000 kwa hekari moja kwa ajili ya kilimo na madebe kumi ya nafaka baada ya mavuno kwa kila hekari moja, huku wafugaji wakilipa takriban shilingi milioni mbili kwa hekari moja katika kipindi cha miezi minne kwa ajili ya kulisha mifugo yao kwenye maeneo ya wawekezaji ambao wamepatiwa vitalu na NARCO kwa mkataba wa kufuga au kulima malisho ya mifugo.

Alifafanua kuwa mkataba wa NARCO na wawekezaji kwa ajili ya kufuga mifugo na kulima malisho hauruhusu wawekezaji kukodisha eneo kwa mtu mwingine kwa ajili ya shughuli zozote kwa kuwa maeneo ya ranchi za taifa ni mali ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO).

Kuhusu deni la zaidi ya Shilingi Bilioni Sita ambalo NARCO inawadai wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi za taifa zilizopo kwenye maeneo mbalimbali nchini, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki ameutaka uongozi wa NARCO kufikia Februari 15 mwaka 2021 saa saba mchana, awe amepata taarifa ya wawekezaji waliolipa madeni yao pamoja na ambao bado hawajalipa, kabla ya kuchukuliwa kwa hatua zaidi.

"Wawekezaji wote ambao tunawadai hapa Usangu na kwenye ranchi zingine wote walipe pesa ya NARCO tulipokubaliana kwenye mkataba tulikubaliana mtalipa pesa, mlipe madeni yenu ifikapo tarehe 15 mwezi februari saa saba mchana muwe mmelipa madeni yenu tunataka NARCO ijiendeshe kibiashara,lakini sioni tukielekea kwenye kujiendesha kibiashara na moja ya matatizo yanayotufanya tusifike huko ni kulea watu wa namna hii," alifafanua Ndaki.

Aliongeza kuwa wale ambao hawatakuwa wamelipa hadi kufikia muda huo wanyang'anywe maeneo hayo ili wapatiwe watu wengine ambao wataweza kulipa kwa mujibu wa mkataba ili NARCO iweze kufikia malengo yake na kulalamika kuwa NARCO imechelewa kuchukua hatua kwa watu ambao wamekuwa na madeni ya siku nyingi.

Alisema kuwa wizara imefanya tathmini juu ya madeni hayo na kuagiza yalipwe katika viwango na tozo mpya zilizowekwa kwa sababu imejiridhisha kwamba kwa gharama hizo NARCO itaweza kujiendesha na kuhudumia vizuri ranchi zake.

Kwa mujibu wa taarifa ya NARCO iliyotolewa na Kaimu Meneja Mkuu wa kampuni hiyo Masele Mipawa, maeneo ya vitalu katika ranchi za taifa yanayokodishwa kwa wawekezaji yamegawanywa katika viwango vitatu, ambapo kiwango cha chini ni Sh.3,500 kwa hekari moja kuanzia eneo lenye hekta 1 hadi 2000, kiwango cha kati ni Sh.5,500 kwa hekari moja kuanzia eneo lenye hekta kuanzia hekta 2001 hadi 5000 na kiwango cha juu ni Sh. 7,500 kwa hekari moja kuanzia eneo lenye hekta zaidi ya 5001.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia), akielekezwa jambo na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel wakati wa kikao na baadhi ya wakulima na wafugaji wanaofanya shughuli zao kwenye Ranchi ya Usangu iliyopo Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya, pamoja na baadhi ya wawekezaji waliopatiwa vitalu katika ranchi hiyo. Waziri Ndaki amefanya ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani humo ili kutambua changamoto zilizopo kwenye Ranchi ya Usangu na kuzitafutia ufumbuzi.** (Picha na Edward Kondela)

Majira 14 Jan 2021, Uk. 10

Scanned with CamScanner